**S.M.Z**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**MTIHANI WA DARASA LA NNE**

**123** **SAYANSI**

**Time: 1:30 Hours.** **SOLUTIONS** **Year: 2018**

---

**MAELEKEZO KWA WATAHINIWA**

**1. Mtihani huu una sehemu MBILI (2) A na B.**

**2. Jibu maswali YOTE katika sehemu A na B.**

**3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**

**4. Majibu YOTE yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.**

**5. Tumia kalamu ya buluu au nyeusi kwa kuandikia na penseli kwa kuchorea tu.**

**6. Simu ya mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.**

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

SEHEMU A: (Alama 40)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

1. Chagua jawabu sahihi kisha andika herufi yake kwenye jadweli hapo chini ya maswali.

   i. Kifaa cha kusafishia chenye mpini

   A. Debe la taka

   B. Glavu

   C. Mopu

   D. Tambara

Jibu sahihi ni C. Mopu. Mopu ni kifaa chenye mpini kinachotumika kusafisha sakafu kwa kufuta uchafu na maji.

ii. Ni lipi kati ya magonjwa yafuatayo silo la kuambukiza?

A. Kisukari

B. Kipindupindu

C. Ukimwi

D. Kifua kikuu

Jibu sahihi ni A. Kisukari. Kisukari ni ugonjwa wa muda mrefu usioambukiza kutoka mtu mmoja kwenda mwingine.

iii. Ukosefu wa madini joto (ayodini) mwilini husababisha

A. Upungufu wa damu mwilini

B. Koromeo la shingo (Goita)

C. Udhaifu wa mifupa

D. Kutoona vizuri

Jibu sahihi ni B. Koromeo la shingo (Goita). Ukosefu wa ayodini husababisha tezi ya shingo kuvimba.

iv. Polio ni ugonjwa unaosababishwa na

A. Bakteria

B. Fangasi

C. Nzi

D. Virusi

Jibu sahihi ni D. Virusi. Polio husababishwa na virusi vinavyoathiri mfumo wa neva.

v. Kati ya wanyama wafuatao ni wepi wasiofugwa?

A. Mbuzi na paka

B. Paa na kobe

C. Punda na ng'ombe

D. Paka na mbwa

Jibu sahihi ni B. Paa na kobe. Hawa ni wanyama wa porini wasiokuwa wa kufugwa majumbani.

2. Andika kweli au sikweli katika jadweli hapo chini.

   i. Faida za misitu ni kupatikana kwa mazao kama asali na nta.

Jibu ni Kweli. Misitu hutoa mazao kama asali, nta na dawa za asili.

ii. Kipigi hupatikana wakati mwangaza wa jua unapopiga katika matone ya maji yanayopatikana angani.

Jibu ni Kweli. Kipigi hutokea mwanga wa jua unapopitia na kuvunjika kwenye matone ya maji.



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

iii. Sauti hutokea katika vitu vilivyo tulia.

Jibu ni Sikweli. Sauti hutokea kutokana na mtetemo wa vitu.

iv. Kipima joto cha maabara hupima jotoridi baina ya nyuzi joto 0°C mpaka 50°C.

Jibu ni Kweli. Kipima joto cha maabara hupima viwango mbalimbali vya joto ndani ya kiwango hicho.

v. Kitalu ni sehemu ndogo iliyopandwa mbegu kwa ajili ya kupata miche.

Jibu ni Kweli. Kitalu hutumika kuoteshea mbegu kabla ya kupandikizwa shambani.

3. Oanisha maelezo ya KIFUNGU A kwa kuchagua neno sahihi kutoka KIFUNGU B. Kisha andika herufi tu kwenye jadweli.

   KIFUNGU A

   i. Eneo linalozungukwa na sumaku

   ii. Ncha za aina moja hukwepana

   iii. Kifaa chenye kuvuta vitu vyenye asili ya chuma

   iv. Njia ya kutengeneza sumaku

   v. Hutumika katika kuonesha uga wa sumaku

KIFUNGU B

A. Sumaku

B. Uga wa sumaku

C. Unga wa chuma

D. Kanuni ya sumaku

E. Kukimbiana

F. Shazia au msumari

G. Kuambukiza

H. Ncha ya kaskazini

i. Jibu sahihi ni B. Uga wa sumaku. Hili ni eneo linalozunguka sumaku.

ii. Jibu sahihi ni E. Kukimbiana. Ncha za aina moja hukwepana.

iii. Jibu sahihi ni A. Sumaku. Sumaku huvuta vitu vya chuma.

iv. Jibu sahihi ni G. Kuambukiza. Ni mojawapo ya njia za kutengeneza sumaku.

v. Jibu sahihi ni C. Unga wa chuma. Hutumika kuonesha uga wa sumaku.

4. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku hapo chini.
   (maradhi, amita, mfinyazi, tepu, kinamo, mafua, kamba, voltimita, mafuta)

a) Potenshali hupimwa kwa kutumia ____________

Jibu ni voltimita. Voltimita hupima tofauti ya potenshali ya umeme.

b) Urefu, eneo, upana na masafa hupimwa kwa kutumia ________________

Jibu ni tepu. Tepu ya kupimia hutumika kupima vipimo mbalimbali.

c) Udongo wa _________________________ ni mchanganyiko wa udongo wa kinongo, kichanga na mboji.

Jibu ni kinamo. Udongo wa kinamo una rutuba nzuri kwa kilimo.

d) Hasara za wadudu ni kusababisha ____________ kwa binadamu.

Jibu ni maradhi. Wadudu husababisha magonjwa kwa binadamu.

e) Kuku huweza kueneza _____________ ya ndege.

Jibu ni mafua. Kuku wanaweza kueneza mafua ya ndege.

SEHEMU B: (Alama 60)
Jibu maswali YOTE kwenye sehemu hii.

5. a) Hewa ina umuhimu gani kwa viumbe?

Hewa ni muhimu kwa viumbe kwa sababu hutumika katika kupumua. Kupitia hewa, viumbe hupata oksijeni inayosaidia uzalishaji wa nishati mwilini. Hewa pia husaidia mimea kutengeneza chakula kupitia usanisinuru.

b) Taja vyanzo viwili (2) vya hewa.

i) Miti. Miti hutoa oksijeni hewani.

ii) Bahari. Bahari huchangia uzalishaji wa hewa safi kupitia viumbe wa majini.

c) Andika matumizi mawili (2) ya hewa.

i) Kupumua kwa binadamu na wanyama.

ii) Kuwasha moto na kusaidia mwako.

6. a) Nini maana ya kivuli?

Kivuli ni eneo lenye giza linalotokea pale mwanga unapozuiliwa kupita na kitu kigumu. Hutokea upande wa pili wa kitu kinachozuia mwanga.

b) Orodhesha vyanzo viwili (2) vya mwangaza visivyo vya asili.

i) Taa ya umeme.

ii) Mshumaa.

c) Taja tabia mbili (2) za mwangaza.

i) Mwanga husafiri kwa mstari ulionyooka.

ii) Mwanga huakisiwa unapogonga uso laini kama kioo.

7. a) Nini maana ya msongo?

Msongo ni hali ya mtu kuwa na mawazo mengi au shinikizo la kihisia linalomfanya ajisikie kuchoka kiakili na kimwili.

b) Andika athari mbili (2) za msongo.

i) Kupungua kwa uwezo wa kufikiri vizuri.

ii) Kuathirika kwa afya ya mwili kama maumivu ya kichwa.

c) Taja dalili mbili (2) za shinikizo la damu.

i) Maumivu ya kichwa mara kwa mara.

ii) Kizunguzungu au kuona kiza.

8. Kamilisha jadweli penye nafasi zilizo wazi.
   a) Mtaro hutumika kupitisha maji machafu.
   b) Reki hutumika kukusanya taka taka.

c) Karo hutumika kupitisha maji machafu.

d) Kibati hutumika kuhifadhia taka.

e) Mafuta ya taa huondoa harufu mbaya chooni.

9. Kamilisha jadweli lifuatalo kwa kujaza maneno sahihi sehemu zilizo wazi.

a) Popo wa Pemba. **dimu** **Nchi kavu**

b) **Tumbili,** **ni adimu** nchi kavu.

c) **Ng'omb**e si adimu na huishi **nchi kavu**.

d) **Kasa** ni si adimu na **huishi baharini.**

e) Pomboo **ni adimu** na **huishi baharini**.

10.a) Jaza sehemu za mmea zilizooneshwa kwa nambari.

1. ua
2. shina
3. mizizi
4. jani
5. Tunda


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

b) Taja kazi moja (1) ya kila sehemu uliyoijaza hapo juu.

1. Mizizi hushikilia mmea ardhini.
2. Shina husafirisha maji na chakula.
3. Majani hutengeneza chakula.
4. Ua hutengeneza mbegu.
5. Tunda hulinda na kusambaza mbegu.